SautiElimu

hakielimu

Toleo la 5
2003/2004

ISSN 0856 8588

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org



Umwambie nini kiongozi wako?

Kutoka kwa mhariri:

Na Rakesh Rajani, Mkurugenzi Mtendaji, HakiElimu

Unafahamu hadithi ya kiongozi mmoja aliyewahi kutembelea kijiji kidogo zaidi, kilichopo mbali sana hapa nchini? Kwa kweli wanakijiji wake walijawa na furaha isiyo kifani lakini walishindwa kuamua waseme nini katika risala yao.

Baadhi yao walitaka kumwambia kiongozi huyo matatizo yanayowakabili, na mbinu za kuyatatua. Lakini wengine wakasema "Hapana!"- Hatutakiwi kumdhalilisha kiongozi wetu, na kwamba ni vizuri kumwonyesha na kumwabia mambo mazuri tu, na kuishukuru Serikali.

Na ndivyo walivyofanya. Walianza kukarabati barabara haraka haraka, walipaka rangi majengo, walifanya kila sehemu ikapendeza. Walidiriki hata kuwaambia watu masikini na walemavu kujificha ili 'wasiharibu ugeni.' Katika hotuba yao walimwambia kiongozi huyo kwamba kulikuwa na maendeleo makubwa na hapakuwa na matatizo yoyote.

Lakini kiongozi huyo alikuwa na busara sana. Aliweza kuona kwamba hotuba ilirembwa na kung'ara kupita kiasi. Hivyo aliamua kuwauliza watu waliokuwa nyuma kabisa ya kundi - wanafunzi, akinamama wazee na mwanaume masikini aliyevaa nguo zenye viraka. Na watu hawa walimwambia ukweli.

Walionyesha sehemu zilizoboreshwa. Walizungumzia pia jinsi kulivyokuwa na matatizo ya kweli. Kuhusu jinsi walivyokosa taarifa walizokuwa wakihitaji. Jinsi gani rasilimali zingeweza kutumika vyema. Namna gani walimu wangeweza kupewa motisha.

Kiongozi aliyashukuru makundi yote mawili. Lakini akasema kwamba licha ya kuridhishwa na nyimbo za kumsifu, aliwashukuru zaidi waliozungumzia matatizo. Akasema kutambua matatizo halisi kwa ukweli na uwazi ni hatua ya kwanza ya kutatua matatizo, kwa manufaa ya wote.

Pengine hii ni changamoto kwa MMEM, mpango wa Serikali wa kuboresha elimu ya msingi. Habari na barua zilizoandikwa katika toleo hili la *SautiElimu* zinasifu mafanikio, lakini zinasisitiza changamoto. Kuwa na matatizo ya utekelezaji ni jambo la kawaida katika mpango mkubwa kama MMEM. Kuhimiza watu kutambua na kufafanua ni hatua ya kwanza ya kuifanya MMEM iwe bora zaidi.

Maalbino wasiwe nyuma katika elimu

Na Sizya Migila, SLP 4505, Dar es Salaam

Kutokana na jamii kukosa elimu ya kutosha kuhusiana na kundi la maalbino na kuendelea kuwabagua, maalbino wengi wameshindwa kushiriki kikamilifu kwa upande wa elimu, kuanzia ya msingi, sekondari hadi elimu ya juu.

Idadi ya maalbino si kubwa miongoni mwa Watanzania, lakini pia idadi ya wanaokwenda shule ni ndogo mno.

Hali hiyo inatokana na kuwepo kwa imani potofu kuanzia ngazi ya familia kuhusu albino. Mathalan, kumekuwa na mitazamo katika jamii kwamba kupata mtoto albino ni mkosi au balaa katika ukoo. Hali hii inajitokeza pale wazazi wanapopata mtoto albino. Mtoto huyo huwa ni chanzo cha migogoro katika familia na mara nyingine husababisha hata kuvunjika kwa baadhi ya ndoa.

Ushauri wangu kwa jamii ni kuwa na mtazamo mpya ambao utasaidia kumuweka albino katika mazingira ya kukubalika katika jamii, kuanzia ngazi ya familia ambayo inategemewa kuwa kiini cha mabadiliko.

Iwapo jamii itamkubali albino, kumthamini na kumpa hadhi kama binadamu wengine, itamsaidia zaidi kujiendeleza na kutoa mchango wake kamili katika jamii. Hivyo basi, kila albino ana haki ya kushiriki kikamilifu katika jamii anayoishi bila kujali mizaha na hisia tofauti dhidi yake. Albino anaweza kushiriki katika mambo yote kwa mfano michezo, fani mbalimbali za sanaa, siasa na shughuli za kujitolea.

Kwa upande wa wazazi au walezi wanawajibika kujitahidi kuwapa moyo maalbino na kutimiza mahitaji yao muhimu, na hasa elimu, ili waweze kujitegemea hapo baadaye. Kundi hili la maalbino likielimika itasaidia kupunguza wimbi la umaskini na kuwafanya waweze kutoa mchango mzuri kwa maendeleo ya taifa.

MMEM isaidie kuvutia wasichana kwenda shule

Na Iddi Makongo, SLP 1028 Mwanza

Naipongeza serikali kwa mpango mzuri wa kuboresha elimu MMEM ambao umeshirikisha wadau wote kwa karibu, katika utekelezaji wake.

Hata hivyo, licha ya juhudi za MMEM kuboresha elimu, bado kuna matatizo ambayo yanawafanya wanafunzi kuendelea kutoroka shule. Baadhi ya matatizo hayo ni umbali kutoka makazi ya wananchi hadi zilipo shule. Mfano, wilayani Serengeti, watoto kuanzia wa shule za chekechea, msingi hadi sekondari hulazimika kutembea mwendo mrefu, takriban kilomita 24 kwenda shule, badala ya kilomita 3 kwa shule za msingi na kwa sekondari kilomita 6. Umbali huo unasababisha shule kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaotoroka.

Matatizo mengine ni kutokuwa na utaratibu wa kutoa chakula cha mchana hasa kwa watoto wanaoishi mbali na shule na ukosefu wa mabomba ya maji kwenye maeneo ya shule. Kukosekana kwa maji shuleni kunawaathiri zaidi wanafunzi wa kike, kwani wanashinda kutwa wakichota maji ya walimu badala ya kuhudhuria masomo darasani.

Wasichana wanakabiliwa na kazi nyingi pia wakiwa nje ya shule. Wengi wao hulazimika kufanya kazi za nyumbani baada ya saa za masomo. Uchovu wa kazi za nyumbani na shuleni huwapunguzia wasichana uwezo kimasomo na kuwafanya hata wakate tamaa ya kwenda shule.

Upungufu wa vifaa nao ni tatizo ambalo humfanya mtoto aamue kutokwenda shule na badala yake kujishughulisha na biashara ndogo ndogo na hasa kufuatia hali ngumu ya uchumi nyumbani. Wengine huamua kufanya kazi za minada, kujiunga na ngoma za asili kama Litungu ambazo zikipita jirani darasa hubaki tupu kwani waliomo hulifuata.

Ili kufanikisha MMEM, serikali kuanzia ya kijiji ishirikiane na kamati za shule na wananchi. Mgawanyo wa fedha za MMEM ufatiliwe kwa makini ili zitumike kubadili mazingira ya shule kuwa bora zaidi na kuwavutia wanafunzi wote, na hasa wa kike.

Ijue MMEM

Na Godfrey Telli, HakiElimu

MMEM ni:

- Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ni programu ya Serikali ya kuboresha elimu ya msingi kwa watoto wote nchini. Hii inajumuisha wasichana na wavulana, matajiri na maskini, pamoja na watoto wenye ulemavu.
- Mpango huu wa kitaifa ni wa miaka mitano, kuanzia 2002 hadi 2006. Shule zote za msingi za Serikali nchini zitafaidika.

Vipengele vikuu:

- ongezeko la uandikishaji,
- kuinua kiwango cha ubora,
- kujenga uwezo,
- matumizi ya fedha na miundo ya kitaasisi

Vipengele vyote vina umuhimu sawa, na vinategemeana. Mpango huu pia unalenga katika masuala muhimu ya jinsia na UKIMWI.

Kuhusu ada na michango:

- Serikali imefuta michango yote ya lazima kwa shule za msingi tangu Januari 2002. Hakuna mtoto atakayezuiwa kuhudhuria shule kwa sababu ya kushindwa kulipa michango. Shule au uongozi wa kijiji hawaruhusiwi kumlazimisha mtu yeyote kulipa fedha kwa elimu ya msingi kwa ajili ya karo, madawati, au kwa ajili ya shughuli nyingine yoyote.
- Wazazi na wanajamii, wanahimizwa kushiriki kikamilifu na kuchangia kwa kadri ya uwezo wao; mchango wowote uwe wa hiari. Jamii inaweza kujitolea nguvukazi katika ujenzi wa nyumba za walimu, vyoo na nyenzo za maji. Wanaweza pia kuwasaidia walimu kwenye shughuli za mitaala ya ziada.

Serikali imefanya hivyo ili kuhakikisha kwamba watoto wote, pamoja na walio masikini, wanapata elimu ya msingi.

Kuhusu majukumu ya kamati ya shule:

- Kuhamasisha, kuhusisha na kuwasilisha habari za elimu kwa wazazi wote, wanafunzi, wadau katika jamii na watendaji na mamlaka za serikali za Mtaa/Kijiji.
- Kushughulikia masuala ya shule ya kila siku, pamoja na utekelezaji wa vipengele vyote vinne vya MMEM.
- Kushirikiana na mwalimu mkuu na walimu wengine kuweka vipaumbele na kuandaa Bajeti na Mipango ya Maendeleo ya shule.
- Kufungua akaunti na kusimamia kwa uhakika na uangalifu fedha zilizo pokelewa kwa ajili ya utekelezaji, kuhakikisha uwajibikaji wa hali ya juu na uwazi katika mchakato unaotumika, ikiwa ni pamoja na kuweka wazi mapato na matumizi kwa jamii.
- Kuandaa na kutoa kwa usahihi na kwa wakati mwenendo na ripoti ya fedha kwa jamii, Kata na Halmashauri.

Jipatie vipeperushi kuhusu MMEM!



Wananchi wote wanatakiwa kufahamu sera ya serikali kuhusu MMEM. Lakini kwa kawaida, taarifa nyingi za kiofisi huandikwa kwa lugha ngumu isiyoeleweka kwa urahisi. Ili kuhakikisha upatikanaji habari katika lugha rahisi, HakiElimu imechapisha vipeperushi 4 kuhusu MMEM.

Marafiki wa Elimu wote pamoja na wengine tunaowatumia nakala ya *SautiElimu* watapata seti moja ya vipeperushi. Iwapo utahitaji zaidi tafadhali tuandikie!

Ukurasa wa 1

SautiElimu

hakielimu

Toleo la 5
2003/2004

ISSN 0856 8588

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Utekelezaji MMEM usiwaache pembezoni walimu

Na Mwalimu Koku Rwehumbiza, Nshambya, Bukoba

Tangu mpango wa MMEM ulipoanza, taarifa nyingi za mafanikio zinaelezea ongezeko la watoto waliosailiwa, madarasa mengi yaliyojengwa na idadi ya walimu walioajiriwa.

Huu ni mwanzo mzuri ingawa wakati huo huo bado kuna malalamiko mengi ya walimu. Baadhi ya malalamiko ni kucheleweshewa au kutolipwa mishahara, kufundisha watoto wengi darasani na kuwa na vipindi vingi katika juma mmoja.

Kwa upande mwingine, mtiririko wa fedha za MMEM haujaeleweka kwa walimu hali inayosababisha utekelezaji wake kuwa mgumu. Katika utekelezaji wa MMEM kwa sasa, suala zima la elimu bora, utoaji elimu bora na mtoaji elimu bora halijitokezi. Maswali ya kujiuliza ni je, elimu bora ni ipi kwa mtazamo wa mtoto, mtazamo wa mzazi, mtazamo wa jamii na taifa? Je, utoaji elimu bora ni upi? Je, tunatarajia mtoaji elimu bora aweje?

Hadi sasa utekelezaji wa MMEM unaelekea kuelemea zaidi kwenye ongezeko la idadi ya wanafunzi na kiasi kidogo kabisa kimewekezwa kwenye ubora wa elimu. Kwa mfano, asilimia 47.8% imewekezwa kwenye majengo ambapo ni asilimia 1.5% tu imewekezwa kwenye kutoa mafunzo kwa kamati za shule na asilimia 1.2% kwenye kutoa mafunzo kwa waalimu.

Kipaumbele kimewekwa kwenye ujenzi wa madarasa kuliko mafunzo na motisha kwa walimu. Mpango uzingatie uwiano mzuri wa vitu vyote hivyo. Kama kuna madarasa mazuri lakini mwalimu anahangaika kufuatilia mafao yake, hana nyumba ya kuishi, ni mgonjwa bima inamzungusha, je atatoa elimu bora?

MMEM inasema kila mwalimu atapewa Dola za Marekani 40 kwa mwaka kwa ajili ya mafunzo. Je, ndivyo ilivyo? Imeelezwa kuwa asilimia 30% ya walimu walio katika mazingira magumu, vijijini na hasa walimu wa kike watajengewa nyumba. Je, hilo limefanyika? Mpango unasema mwalimu asifundishe zaidi ya masaa 20 kwa juma. Akifanya hivyo kuna malipo za ziada. Je, yako wapi? Walimu wanaoshiriki na watakaoshiriki MEMKWA watalipwa? Je, wamelipwa? Utekelezaji wa MMEM usielemee kwenye ujenzi wa madarasa pekee!

MMEM itilie mkazo upatikanaji wa habari

Na Mary Nsemwa, HakiElimu

Mambo mengi mazuri yamefanyika tangu kuanzishwa kwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Baadhi ya mambo hayo ni ujenzi wa madarasa, kuongeza uandikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule na kuajiri walimu wapya.

MMEM inalenga kuinua kiwango cha elimu kwa kushirikisha wadau wote katika utekelezaji wake, wakiwemo wanafunzi, walimu, wazazi, Serikali, taasisi mbalimbali na wahisani.

Swali la kujiuliza ni kuwa jukumu la wadau mbalimbali ni lipi katika utekelezaji wa MMEM? Wanapataje habari za elimu? Je, wadau hao wanatimizaje wajibu wao? Kiini cha mabadiliko katika elimu ni wanafunzi, walimu na wazazi. Lakini je, ushiriki wao unaridhisha? Mara nyingi makundi haya matatu yamekuwa hayafahamu nini kinaendelea kuhusu sera na mipango ya elimu.Wamekuwa, wakipokea maagizo kutoka ngazi ya juu tu.

Hata wanapopata habari zinakuwa hazieleweki au zinawachanganya kutokana na jinsi zilivyotolewa na viongozi mbalimbali kwa nyakati tofauti. Mathalan, katika utafiti mmoja, baadhi ya walimu na wanafunzi waliowahi kuulizwa maana ya MMEM walijibu kuwa ni ujenzi wa madarasa ama ni kuhimiza walimu kujiendeleza, na si zaidi ya hapo.

Kwa ujumla, wananchi wanahitaji kupata habari ili wajue haki zao na waweze kuwajibika kwa kushirikiana na serikali yao. Mabadiliko ya elimu nchini yatakuwepo iwapo habari zitawafikia wadau wote, na kwa wakati muafaka.



HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki za binadamu na demokrasia katika elimu kwa kuwezesha jamii kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera za elimu, kuimarisha ubunifu wa uendeshaji wa mijadala na midahalo ya umma, kufanya utafiti yakinifu, wenye kuhoji, wenye kuchambua, kutetea na kushirikisha wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yeyote ya jarida hili kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala kwa HakiElimu.

ISSN 0856 8588

© HakiElimu, 2003

Mhariri Mkuu: Rakesh Rajani
Timu ya *SautiElimu*: Lilian R. Kallaghe, Mary Nsemwa na Godfrey Telli
Mchoraji: Marco Tibasima
Picha: Japhet Makongo

Tuandikie!
SautiElimu
SLP 79401
Dar es Salaam
Simu: 022 2151852 / 3
Faksi: 022 2152449
Baruapepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org



Ukurasa wa 2

Barua kwa SautiElimu



Mhariri,
Napenda kuwapongeza wadau wa elimu waliokaa na kujadili kuanzishwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na kufuta michango yote shuleni.

Kwa kweli michango ilikuwa kero miongoni mwa wazazi hususan kipindi cha kuandikisha watoto kuanza darasa la kwanza. Wazazi wenye uwezo ndio waliokuwa wakipeleka watoto wao shule.

Pamoja na kufurahia mpango huo, wazazi tumeanza kupata wasiwasi juu ya upatikanaji wa elimu bora kwa watoto wetu. Wanafunzi wamekuwa wengi mno madarasani hali inayosababisha watoto wasielewe wanachofundishwa.

Badala ya kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo kwa manufaa ya watoto wote, baadhi ya walimu wameanzisha mafunzo ya ziada (tuition). Mafunzo haya kwa kweli yanawanufaisha watoto wa wazazi wenye uwezo pakee. Nashauri mafunzo hayo yatolewe bure kwa wanafunzi wa darasa la saba hasa vijijini ili kila mtoto apate elimu bora bila kubaguliwa.

Jovenary Edward
SLP 1168
Bukoba

•••

Mhariri,
Naipongeza Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) kwa kuanza kutoa semina kwa kamati za shule kuhusu namna ya kuendesha shule.

Kwa kweli wananchi katika eneo letu walifurahia sana mafunzo. Pamoja na hayo tunapendekeza serikali ichapishe na kusambaza miongozo mahsusi ya namna ya kuendesha shule na mengine yanayohusu uboreshaji elimu kwa ujumla.

Tunaipongeza MMEM kwa mafanikio yake hasa katika uwazi na uwajibikaji.

Wilix Mahenge
SLP 1226
Iringa

•••

Mhariri,
Naomba nitoe ushauri wangu kuhusu elimu ya msingi hasa katika somo la stadi za kazi.

Somo hili lenye fani za ufundi umeme, useremala, uchoraji, muziki na michezo ni bora kwa kuwaandaa wanafunzi ili waweze kujiajiri baada ya kuhitimu shule ya msingi.

Inasikitisha kuona kwamba watoto hawafundishwi kwa vitendo kutokana na walimu wengi kutokuwa na utaalamu wa kutosha katika somo hilo.

Vilevile walimu wapya ambao wamepitia mtaala huo wanakiri kuwa hawakupatiwa mafunzo ya kutosha wakiwa vyuoni. Nashauri serikali itoe mafunzo hata ya muda mfupi kwa wakufunzi wa vyuo vya walimu na walimu wa shule za msingi ili somo hilo lifundishwe ipasavyo.

Flora Mpombo
SLP 3080
Mbeya

Mhariri,
Tumefurahi kwamba serikali imefuta karo na michango yote kwa shule za msingi ili kila mtoto aweze kupata elimu bure.

Hata hivyo, serikali pia ingempunguzia mzazi gharama za kununua vitabu, madaftari na za kuchapa mitihani kwa kuhakikisha kwamba ruzuku ya Dola za Marekani 10 zilizotengwa kwa kila mwanafunzi zinafika shuleni kwa wakati na kiwango kinachotakiwa.

Takriban asilimia 81 ya Watanzania wana hali ngumu kiuchumi. Familia nyingi zinashindwa kutoa hata yale mahitaji muhimu, hali inayowaathiri watoto kisaikolojia.

Kwa kutoa fedha hizo shuleni kwa wakati, mzazi atabaki na jukumu la kugharamia sare za shule na kuwafanya watoto wote, bila kujali uwezo wa familia, kuwa nadhifu na kujisikia vyema wawapo katika mazingira ya shule. Wanafunzi pia wataepuka adhabu zinazotolewa na baadhi ya walimu pindi wanapokosa ama sare au kushindwa kuchangia ununuzi wa karatasi za mitihani!

John Frederick
c/o Mary Kidola Masolwa
SLP 11133
Mwanza

•••

Mhariri,
Miaka karibu 15 iliyopita, wazazi wengi walishindwa kuwapeleka watoto wao shule kutokana na kushindwa kulipa ada na michango mingine.

Sababu nyingine za wazazi kutowapeleka watoto wao shule, hasa wa darasa la kwanza, ilikuwa ni pamoja na umbali kutoka yalipo makazi ya watu.

Naipongeza Serikali kwa kushirikiana na wananchi kujenga shule nyingi za msingi karibu na maeneo wanayoishi watu hasa vijijini. Vilevile napongeza hatua ya kuondoa michango yote shuleni isipokuwa ile ya hiari.

Hivi sasa hakuna sababu kwa wazazi kushindwa kuwapeleka watoto wao shuleni. Nashauri Serikali itoe adhabu kwa wazazi watakaoshindwa kuwaandikisha watoto wao shule au kuwakatiza masomo ili iwe fundisho kwa wengine. Watoto wote wana haki ya kupata elimu bora bila kubaguliwa, wawe masikini au matajiri.

Jamila Ramadhani Nangay
SLP 1411
Zanzibar

•••

Mhariri,
Napenda kuelezea kero ambazo bado zinatukabili katika shule yetu.

Kwanza, wanafunzi bado tunakaa chini, vitabu na madawati hayatoshi na mazingira ya shule kwa ujumla hayaridhishi, hasa upande wa vyoo na mashimo ya taka.

Licha ya kufutwa ada, bado kuna michango ya mara kwa mara. Je, hiyo elimu bora tutaipataje katika mazingira haya? Viongozi wa elimu mkoani hapa mko wapi? Tunaomba viongozi mshirikiane na jamii kutuondolea kero hizi. Msipofanya hivyo elimu yetu itaendelea kushuka!

Mwanafunzi
SLP 144
Igoma
Mwanza

Tuboreshe SautiElimu

Tunatafuta maoni kuhusu namna ya kuboresha jarida hili. Je, ungependa tuendelee na mpangilio huu wa bango la kubandika ukutani au mfumo wa kijitabu? Tufanye nini ili kuliboresha zaidi na kukuwezesha kulisoma kwa urahisi? Kama una maoni tuandikie!' Atakayetoa maoni bora atapewa zawadi ya fulana ya HakiElimu!

